TAARIFA YA TATHMINI YA MATOKEO YA MTIHANI WA KUHITIMU ELIMU YA MSINGI (PSLE) MWAKA 2022 KWA MKOA WA PWANI

1.0 UTANGULIZI

Katika Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi PSLE 2022 Mkoani Pwani, jumla ya shule 645 zilishiriki Mtihani huo. Shule zilizopata matokeo ni shule 644 na Shule 1 ilifungiwa. Aidha wanafunzi waliosajiliwa kufanya mtihani huo ni **47,906** wakiwemo wasichana **24,292** na wavulana **23,614**. Jumla ya wanafunzi **47,453** (wavulana **23,333** na wasichana **24,120**) sawa na **99.05%** walifanya mtihani. Wanafunzi **453** (wavulana **281** na wasichana **172**) sawa na asilimia **0.94%** hawakufanya mtihani kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Utoro, vifo na ugonjwa.

Jumla ya wanafunzi **39,463** wakiwemo wavulana **19,159** na wasichana **20,304** sawa na asilimia **83.162%** walifaulu mtihani huo. Aidha watahiniwa **7,990** (wavulana **4,174**, wasichana **3,816**) ambao ni sawa na asilimia **16.838%** hawakufaulu.

2.0 TAARIFA YA TATHMINI YA MATOKEO KIMKOA

Hali ya Ufaulu katika Mkoa wa Pwani kwa mwaka 2022 ni asilimia **83.162%**

4.0 UFAULU WA KIMASOMO

Hali ya matokeo ya mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi PSLE 2022 ni kama ifuatavyo katika jedwali namba 2. Aidha ufaulu unatofautiana kwa asilimia vaina ya somo moja na lingine.

Jedwali 2: Hali ya Ufaulu kwa Kila Somo

NA	SOMO	JINSI	MADARAJA YA UFAULU									
			A	B	C	A-C	%	D	E	D-E	%	WALIOFANYA
	HISABATI	WAV	780	2264	9935	12979	54.96	10243	293	10536	44.62	23614
		WAS	681	1978	9895	12554	51.68	11083	286	11369	46.80	24292
1		**JUMLA**	**1461**	**4242**	**19830**	**25533**	**53.30**	**21326**	**579**	**21905**	**45.72**	**47906**
	ENGLISH	WAV	1064	1203	6094	8361	35.41	14426	629	15055	63.75	23614
		WAS	1104	1072	6485	8661	35.65	14665	698	15363	63.24	24292
2		**JUMLA**	**2168**	**2275**	**12579**	**17022**	**35.53**	**29091**	**1327**	**30418**	**63.50**	**47906**
	KISWAHILI	WAV	7479	9279	3987	20745	87.85	1991	573	2564	10.86	23614
		WAS	7700	9869	4346	21915	90.21	1712	442	2154	8.87	24292
3		**JUMLA**	**15179**	**19148**	**8333**	**42660**	**89.05**	**3703**	**1015**	**4718**	**9.85**	**47906**
	MAARIFA YA JAMII	WAV	1633	6011	9767	17411	73.73	5354	525	5879	24.90	23614
		WAS	1441	5384	11383	18208	74.95	5575	387	5962	24.54	24292
4		**JUMLA**	**3074**	**11395**	**21150**	**35619**	**74.35**	**10929**	**912**	**11841**	**24.72**	**47906**
	URAIA NA MAADILI	WAV	1077	8689	7508	17274	73.15	3442	703	4145	17.55	23614
		WAS	956	10594	9211	20761	85.46	3190	611	3801	15.65	24292
5		**JUMLA**	**2033**	**19283**	**16719**	**38035**	**79.40**	**6632**	**1314**	**7946**	**16.59**	**47906**
	SAYANSI	WAV	1288	5037	10815	17140	72.58	5748	408	6156	26.07	23614
		WAS	1044	4630	11829	17503	72.05	6331	323	6654	27.39	24292
6		**JUMLA**	**2332**	**9667**	**22644**	**34643**	**72.31**	**12079**	**731**	**12810**	**26.74**	**47906**

5.0 TATHMINI YA ALAMA ZA UFAULU KWA KILA SOMO

Hali ya matokeo ya mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi PSLE 2022 inaonesha kuwa wanafunzi wamefanya vizuri katika somo la Kiswahili kwa asilimia **89.05%** na wamepata ufaulu wa chini katika somo la English kwa asilimia **35.53%.** Ufaulu kwa masomo mengine ni kama ifuatavyo Uraia na Maadili (**79.40**%), Sayansi na Teknolojia (**72.31%),** Maarifa ya Jamii (**74.35%)** na Hisabati (**53.30%).** Matokeo ni kama inavyonekana katika jedwali hapo chini

7.0 MIKAKATI YA KUBORESHA UFAULU

Kutokana na matokeo ya mwaka 2022 kushuka, Mkoa wa Pwani umeweka mikakati ifuatayo ili uweze kuinua kiwango cha ufaulu.

i. Kufanyika kwa mitihani ya Utamilifu Mkoa kwa watahiniwa tarajali ili kuwajengea uwezo na ari ya kujifunza zaidi.
ii. Kuhakikisha kuwa kila Afisa Elimu Kata anaratibu ufanyikaji wa mitihani ya Upimaji isiyopungua mitatu ndani ya kata yake kwa madarasa yenye watahiniwa tarajali.
iii. Kuhakikisha kuwa Walezi wa Kata wanafuatilia kwa karibu mazoezi ya upimaji katika maeneo yao wanayolea ili kupata taarifa zenye uhalisia katika upimaji.
iv. Kuhakikisha kuwa kila Afisa Elimu Kata na Walimu Wakuu wanaratibu na kusimamia mitihani ya kila Mwezi (Monthly test) katika shule zilizopo katika maeneo yao ya kazi.
v. Kuhakikisha kuwa kila Halmashauri ina mikakati ya kuondoa alama D na E katika mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.Hivyo kuwe na msisitizo katika kuondoa changamoto ya KKK katika shule husika.
vi. Kuhakikisha kuwa Maafisa Elimu Kata na Walimu Wakuu wanaimarisha na kusimamia ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya shule. Hivyo wahakikishe uwepo wa maandalizi ya ufundishaji kwa walimu yaani maazimio ya kazi, maandalio ya somo,zana za kufundishia na kujifunzia na nukuu za somo kwa kila mwalimu kabla na wakati wa kufundisha.
vii. Kuhakikisha kuwa mamlaka za serikali za vijiji na Kata zinashirikishwa kikamilifu katika kushughulikia masuala ya utoro wa wanafunzi ili kuimarisha mahudhurio yao shuleni.
viii. Kuhamasisha jamii kuchangia chakula kwa ajili ya wanafunzi ili kupambana na changamoto ya mahudhurio ya wanafunzi shuleni.
ix. Kuimarisha ushirikiano wa walimu, wazazi na wanafunzi shuleni
x. Kuhakikisha kuwa walimu wanajengewa uwezo wa Kitaaluma na kitaalamu kwa kutumia walimu mahiri na wadau wengine wa Elimu.
xi. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa Halmashauri kuweka kwenye bajeti fedha za ujenzi wa miundombinu.
xii. Halmashauri kuendelea kutenga kwenye bajeti zao na kushirikisha wananchi na wadau mbalimbali kujenga miundombinu ya shule kulingana na mahitaji;

xiii. Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri zake kuendelea kuomba vibali vya ajira mbadala na pia kuendelea kusimamia nguvu kazi ya rasilimali chache iliyopo ili kuendelea kupata matokeo yenye tija.

8.0 HITIMISHO

Mkoa wa Pwani utasimamia utekelezaji wa mikakati iliyopangwa ili kuinua kiwango cha ufaulu. Aidha, Viongozi wa Elimu katika ngazi za Shule, Kata, Halmashauri na Mkoa, wanaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa majukumu, kufanya tafiti za kitaaaluma pamoja na kuwa na uwajibikaji wa pamoja katika suala zima la kuboresha Elimu.